



Asili : **Kiingereza**

N° : **ICC-01/04-01/12**

Tarehe : **13 mwezi ya saba 2012**

**CHUMBA CHA UTANGULIZI II**

Inaundwa na : **Bibi jije Ekaterina Trendafilova, jije prezida  
Bwana jije Hans-Peter Kaul  
Bwana jije Cuno Tarfusser**

**HALI MU JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO  
AFERE YA *PROKIRERE NA SYLVESTRE MUDACUMURA***

**Ni yenye batu bote banaweza kuona na yenye mulivutwa maneno  
Uamuzi kutokana na ombi yenye Prokirere alifanya kulingana na **artikle 58****

Uamuzi wa kujulisha watu hawa, kufuatana na kanuni 31 ya Kanuni za Mahakama :

**Biro ya Prokirere**

Bibi Fatou Bensouda, Prokirere

**Avoka wa utetezi**

**Benye kusimamia baviktime mbele ya sheria**

Benye kusimamia baombaji mbele ya sheria

**Baviktime benye habana mtu wa kubasimamia**

**Baombaji benye habana mtu wa kubasimamia (kushiriki/malipo)**

**Biro ya ushauri ya umma ya baviktime**

**Biro ya ushauri ya umma ya utetezi**

**Benye kusimamia mainchi**

*Amicus curiae*

**Bengine**

#### **BIRO YA GREFYE**

---

**Grefye na makamu wa Grefye**

Bibi Silvana Arbia, Grefye

Bwana Didier Preira, makamu wa Grefye

**Tawi la msaada ku Utetezi**

**Kitengo ya msaada ku baviktime na batemwe**

**Tawi ya zuizi**

**Kitengo ya kushiriki ya baviktime na cha malipo**

**Bengine**

## Yaliyomo

I.Uwezo wa kisheria wa Mahakama na kukubaliwa kwa afere .....	6
A.Uwezo wa kisheria wa Mahakama .....	6
B. Kukubaliwa kwa afere .....	9
II. Je,Kuna sababu za kutosha ya kuamini kwamba jinai moja ao nyingi zenye kupatikana katika ombi ya Prokirere ilitendeka ? .....	9
A. Jinai dhidi ya ubinadamu .....	10
B. Jinai za kivita .....	13
1) Alama za hali za jinai ya kivita .....	13
2) Matendo yenye kuunda jinai zenye zilitendwa katika hali ya vita isiyokuwa ya kimataifa ao zilizotendwa kwa uhusiano na hali hii .....	16
3) Kwa kumaliza .....	24
III. Kweli, kuna sababu zakutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anabeba muzigo ya jinai zenye kupatikana katika ombi ya Prokirere ?.....	25
IV. Mafaa ya kumufunga Sylvestre Mudacumura kufuatana na artikle 58-1-b ya Mkatoba .....	30
V. Kwa kumaliza .....	32

**CHUMBA CHA UTANGULIZI II** (« Chumba ») ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (« Mahakama») inatoa uamuzi juu ya ombi yenye ilitolewa kufuatana na article 58 (« Ombi ya Prokirere » ao « Ombi »)<sup>1</sup> ; Ombi ya Prokirere<sup>2</sup> ya kutoa manda ya kumukamata Sylvestre Mudacumura.

1. Tarehe 3 mwezi ya tatu 2004, hali katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) kwenye afere ya Sylvestre Mudacumura inatokea, ililetwa kwa Prokirere na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kufuatana na artikle 13-a na 14 ya Mkataba wa Roma (« Mkataba »)<sup>3</sup>.
2. Tarehe 17 mwezi ya sita 2004, Prokirere alimujulisha Prezida wa Mahakama ya kwamba kuna msingi wa kutosha kwa kuanza ankete katika hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo<sup>4</sup>.
3. Tarehe 6 mwezi ya saba 2004, Biro ya Prezida ilipatia hali katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa Chumba cha utangulizi I<sup>5</sup>.
4. Tarehe 15 mwezi ya tatu 2012, Biro ya Prezida ilipatia tena hali katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa Chumba cha utangulizi II<sup>6</sup>.
5. Tarehe 15 mwezi ya tano 2012, Prokirere aliomba manda ya kukamata itolewe kwa Sylvestre Mudacumura (« Ombi ya kwanza»)<sup>7</sup>.

---

<sup>1</sup> ICC-01/04-616-Conf-Exp na nyongeza zake. Kuangalia pia "Public Redacted Version of Prosecutor's Application under article 58", ICC-01/04-616-Red.

<sup>2</sup> Tarehe 15 mwezi wa sita 2012, Fatou Bensouda alikula kiapo kama Prokirere wa mupya wa Mahakama.

<sup>3</sup> Barua ya tarehe 3 mwezi wa tatu 2004 kwenye Joseph Kabila alitumaka ku CPI hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, yenye iliongezewa ku "Prosecutor's Application for Warrants of Arrest, Article 58 ", ICC-01/04-98-US-Exp-Anx1.

<sup>4</sup> Barua yenye ilitumiwa na Prokirere tarehe 17 mwezi wa sita 2004 kwa Prezida wa Mahakama, yenye iliongezewa ku "Decision Assigning the Situation in the Democratic Republic of Congo to Pre-Trial Chamber I", ICC-01/04-1, p. 4.

<sup>5</sup> Biro ya Prezida, "DECISION ASSIGNING THE SITUATION IN THE DEMOCRATIC REPUBLIC OF THE CONGO TO PRE-TRIAL CHAMBER I", ICC-01/04-1.

<sup>6</sup> Biro ya Prezida, *Decision on the constitution of Pre-Trial Chambers and on the assignment of the Democratic Republic of the Congo, Darfur, Sudan and Côte d'Ivoire situations*, ICC-01/04-02/06-32.

6. Tarehe 31 mwezi ya tano 2012, Chumba ilitupilia mara moja ombi ya kwanza ya Prokirere juu ya kukosa kupana mwangaza<sup>8</sup>.

7. Tarehe 13 mwezi ya sita 2012, Prokirere alitoa ombi kwa Chumba katika maneno yafuatayo:

[TAFSIRI] 1. Kuona ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo wa kutenda jinai za kivita, na jinai dhidi ya ubinadamu zenye ziko ndani ya uwezo wa kisheria ya Mahakama na zenye zilitendedwa na baFDLR katika majimbo ya Nord-Kivu na Sud-Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) katikati ya tarehe 20 mwezi ya kwanza 2009 na mwisho wa mwezi ya kenda 2010, kufuatana na artikle 25-3-a ya Mkataba ao pia kufuatana na artikle 25-3-b ao artikle 28-a ya Mkataba;

2. Kuamua ya kwamba kukamatwa kwa Sylvestre MUDACUMURA ni ya lazima ;

3. Kutoa manda ya kumukamata Sylvestre MUDACUMURA;

4. Kuamuru Biro ya Grefye itayarishe na itume kwa wakubwa viongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ombi ya kumukamata Sylvestre MUDACUMURA na kumupana, yote ikizungumza na kushirikiana na Biro ya Prokirere ;

[IMEVUTWA].<sup>9</sup>

8. Kwa kuamua juu ya ombi ya Prokirere, Chumba itaangalia vizuri: i) uwezo wa kisheria wa Mahakama na kukubaliwa kwa afere; ii) kujua kama kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba moja ao mingi ya zile jinai zenye zinatajwa katika ombi ya Prokirere ilitendwa; iii) kama kuna sababu za kutosha za kuamini ya kwamba Sylvestre Mudacumura alitenda jinai zenye zinaandikwa katika ombi ya Prokirere; na iv) kama byote byenye binafaa juu ya kutoa manda ya kumukamata Sylvestre Mudacumura binaenea.

<sup>7</sup> ICC-01/04-612-Conf-Exp, "Corrigendum to 'Public redacted version of Prosecution's Application under Article 58' ", ICC-01/04-612-Red-Corr na nyongeza.

<sup>8</sup> Chumba cha utangulizi II, "Decision on the Prosecutor's Application Under Article 58", ICC-01/04-613.

<sup>9</sup> Ombi ya Prokirere, ukurasa (*hapa chini « uk. »*) 57 na 58.

## I.Uwezo wa kisheria wa Mahakama na kukubaliwa kwa afere

### A.Uwezo wa kisheria wa Mahakama

9. Artikle 19-1 ya Mkataba inasema hivi: « Mahakama inaangalia kama kweli iko na uwezo wa kisheria ya kusambisha kila afere yenye inaletwa mbele yake. Mahakama inaweza palepale kusema kama afere inaweza kukubalika kufuatana na artikle 17. » Kwa hiyo, kujua kama afere ya Sylvestre Mudacumura iko ndani ya uwezo wa kisheria ya Mahakama ni sharti ya kwanza kwa kutoa manda ya kumukamata<sup>10</sup>.

10. Ili jinai ikuwe ndini ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, inafaa sharti hizi zitimizwe :  
i) inafaa jinai ikuwe moja kati jinai zenye zinatajwa ku artikle 5 ya Mkataba (uwezo wa kisheria *ratione materiae*) ; ii) inafaa jinai itendwe kati ya muda yenye iliandikwa ku Artikle 11 ya Mkataba (uwezo wa kisheria *ratione temporis*) ; na iii) inafaa jinai itimize sharti zote zenye zinaandikwa ku artikle 12 ya Mkataba. Maana yake inafaa jinai itendeke wala katika moja kati ya Nchi zinazounda Mahakama ao itendwe na basivile kutoka moja kati ya Nchi zinazounda Mahakama, ao inchi ama basivile ya inchi yenye ilitoa tamko inayoandikwa ku artikle 12-3 ya Mkataba<sup>11</sup>. Uamzi kuhusu sharti zile tatu ilitangazwa na Chumba kutokana na ombi pia kutokana na ushahidi ao habari zingine zenye zilitolewa na Prokirere.

11. Kuhusu sharti ya kwanza, Chumba inaamini ya kwamba jinai yenye Sylvestre Mudacumura anashtakiwa ni jinai zenye zinaandikwa katika Mkataba na kwamba sharti ya kwanza kuhusu uwezo wa kisheria *ratione materiae* inatimizwa.

12. Kuhusu sharti ya pili, ni kusema uwezo wa kisheria *ratione temporis* ya Mahakama, Chumba ina kumbusha ya kwamba Mkataba ilianza kutumika katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo tarehe 1 mwezi ya saba 2002. Chumba inaona wazi ya kwamba jinai zenye zinatajwa zilitendwa nyuma ya tarehe 1 mwezi ya saba 2002, hasa kati ya

<sup>10</sup> Chumba cha utangulizi III, "Décision relative à la Requête du Procureur aux fins de délivrance d'un mandat d'arrêt à l'encontre de Jean-Pierre Bemba Gombo," ICC-01/05-01/08-14, par. 11.

<sup>11</sup> Chumba cha utangulizi III, "Décision relative à la Requête du Procureur aux fins de délivrance d'un mandat d'arrêt à l'encontre de Jean-Pierre Bemba Gombo," ICC-01/05-01/08-14, par. 12.

tarehe 20 mwezi ya kwanza 2009 na mwisho wa mwezi ya kenda 2010. Kwa hiyo sharti ya pili inatimizwa.

13. Kuhusu sharti ya tatu, maana yake njia zingine zinazoandikwa kwa artikle 12 ya Mkataba, Chumba inaamini ya kwamba jinai zenye Sylvestre Mudacumura anashitakiwa zilitendwa katika eneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kwa hiyo Chumba inaamua ya kwamba sharti ya tatu inatimizwa.

14. Chumba inakumbusha tena ya kwamba « afere ya kutokana na ankete juu ya hali fulani itakuwa ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama tuu, ikiwa kama jinai za ile afere hazipite mipaka ya eneo na ya wakati. Pia haziwezi kupita mipaka ya kipekee yenye inahusu hali ya ile ankete, na yenye kupatikana ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama<sup>12</sup> ». “ *Parametres*” za ankete ya hali moja zinaweza kuhusu jinai zenye zilitendwa mbele ao zenye zilikuwa karibu ya kutendwa wakati afere ililetwa ku Mahakama. Pia zinahusu jinai zenye zilitendwa nyuma, kama tuu ziko zinaambatana kabisa na hali ya mwanzo wakati afere ililetwa ku Mahakama<sup>13</sup>.

15. Kwa hiyo, hali katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kwenye afere ya Sylvestre Mudacumura inatoka, ilipelekwa kwa Prokirere kupitia barua ya tarehe 3 mwezi ya tatu 2004. Mu ile barua, Raisi Joseph Kabila alimuombaka Prokirere afanye ankete juu ya « hali katika inchi [y]ake tangu tarehe 1 mwezi ya saba 2002, ambako kulizaniwa ya kwamba jinai zenye ziko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai

<sup>12</sup> Chumba cha utangulizi III, “*Décision relative à la Requête du Procureur aux fins de délivrance d’un mandat d’arrêt à l’encontre de Jean-Pierre Bemba Gombo*”, ICC-01/05-01/08-14, par. 12 ; Chumba cha utangulizi I, “*Decision concerning Pre-Trial Chamber I’s Decision of 10 February 2006 and the Incorporation of Documents into the Record of the Case against Mr Thomas Lubanga Dyilo*”, ICC-01/04-01/06-8-Corr, annex 1, para. 21 (inayokuwa na Uamuzi juu ya ombi ya Prokirere kwa kutoa manda ya kumukamata Thomas Lubanga Dyilo, ombi yenye ilitolewaka mbele, maana yake tarehe 10 mwezi wa pili 2006).

<sup>13</sup> *Angalia* Chumba cha utangulizi I, “*Decision on the Defence Challenge to the Jurisdiction of the Court*”, ICC-01/04-01/10-451, para. 21 ; Chumba cha utangulizi I, “*Decision on the Prosecutor’s Application for a Warrant of Arrest Against Callixte Mbarushimana*”, ICC-01/04-01/10-1, para. 6 (enye ililnawa tarehe 28 mwezi wa kenda 2010) ; Chumba cha utangulizi III, “*Corrigendum to ‘Judge Fernandez de Gurmendi’s separate and partially dissenting opinion to the Decision Pursuant to Article 15 of the Rome Statute on the Authorisation of an Investigation into the Situation in the Republic of Côte d’Ivoire’*”, ICC-02/11-15-Corr, paras 70-72 (mawazo ya kipekee na ya kupinga kwa kipande tuu kutoka kwa Jije Fernández de Gurmendi).

zilitendeka<sup>14</sup> ». Tarehe 17 mwezi ya sita 2004, Prokirere alimujulisha Prezida wa CPI kwamba kufuatana na sharti zote zenye zinaandikwa ku artikle 53 ya Mkataba, kuna msingi wa kutosha kwa kuanza ankete<sup>15</sup>. Alifasiria kama hali yenye ankete inahusu iko katika eneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo tangu tarehe 1 mwezi ya saba 2002<sup>16</sup>.

16. Ombi ya Prokirere inaangalia jinai zenye zinawaziwa kutendwa kati ya mwezi ya kwanza 2009 na mwisho wa mwezi ya kenda 2010 katika hali ya vita ku majimbo za Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo). Kiisha kuchunguza habari za kutoka kwa Prokirere, Chumba inaamini ya kwamba tangu tarehe 4 mwezi ya kumi na mbili 2002 ao mbele ya pale, mapambano ilikuwa kati ya majeshi ya taifa na makundi yenye silaha pale mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, sana sana katika majimbo ya Kivu na ya Ituri<sup>17</sup>. Chumba ina uhakika pia ya kwamba tangu wakati afere ililetwa mbele yake ao mbele kidogo, ba *Forces démocratiques pour la libération du Rwanda* (FDLR) baliendesha matendo ya kijeshi katika mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika matendo ile, FDLR balifanya jinai zenye ziko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama<sup>18</sup>. Njo maana Chumba inaona wazi ya kwamba afere inamuhusu Sylvestre Mudacumura inahusiana kupelekwa kwa hali ile ya Kidemokrasia ya Kongo yenye ililetwa mbele ya Mahakama.

17. Kutokana na maneno yenye inaandikwa hapa juu na kwa msingi wa ushahidi na habari Prokirere alitoa, Chumba inaamua ya kwamba afere ya Sylvestre Mudacumura iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama.

<sup>14</sup> Barua ya tarehe 3 mwezi wa tatu 2004 kwenye Joseph Kabila alituma ku CPI hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, yenye ilisindikiza maandishi ya nyongeza ya "Prosecutor's Application for Warrants of Arrest, Article 58, ICC-01/04-98-US-Exp-Anx1.

<sup>15</sup> *Angalia* Biro ya Prezida, "DECISION ASSIGNING THE SITUATION OF THE DEMOCRATIC REPUBLIC OF CONGO TO PRE-TRIAL CHAMBER I", ICC-01/04-1, p. 4.

<sup>16</sup> Kuangalia matangazo ya kupasha habari ya tarehe 23 mwezi wa sita 2004. The Office of the Prosecutor of the International Criminal Court opens its first investigation, ICC-OTP-20040623-59.

<sup>17</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 9, Uk. 5, 10, 15 na 19. *Kuangalia pia* Chumba cha utangulizi I, "Decision on the Prosecutor's Application for a Warrant of Arrest Against Callixte Mbarushimana", ICC-01/04-01/10-1, par. 6 -7.

<sup>18</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 9, Uk. 8 mpaka 10, 15, 19, 21 na 22.



## B. Kukubaliwa kwa afere

18. Kufuatana na msemwa wa pili wa artikle 19-1 ya Mkataba, Mahakama « inaweza mara moja kuamua kama afere inakubaliwa kufuatana na atikle 17 ». Chumba haione kama ni lazima kuchunguza kwa sasa kama afere<sup>19</sup> inaweza kukubaliwa ao hapana.

## II. Je, Kuna sababu za kutosha ya kuamini kwamba jinai moja ao nyingi zenye kupatikana katika ombi ya Prokirere ilitendeka ?

19. Kuhusu ma sharti ya kutumia mtu manda ya kumukamata, artikle 58-1 ya Mkataba inasema ya kwamba inafaa tuu Chumba iwe na uhakika ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba mtu alitenda jinai yenye iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama. Inatosha tu ushahidi isaidie kuamini ya kwamba mtu alifanya jinai yenye iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama. Si lazima uamuzi uwe uamuzi pekee wenye kutoka kwa ushahidi uliotolewa<sup>20</sup>.

20. Chumba inaona ya kwamba Ombi ya Prokirere ina maneno mingi yenye kufanana na dosye katika afere ya *Prokirere c. Callixte Mbarushimana*. Chumba cha utangulizi ilikatalaka kwa uwingi wa bajije kuhakikisha mashtaka katika ile afere<sup>21</sup>. Uamuzi yao ilikubaliwa na Chumba cha rufaa<sup>22</sup>. Lakini Chumba inaona ya kwamba uamuzi yenye ilikamatiwa na Chumba cha utangulizi kwa kuhakikisha mashtaka juu ya Callixte Mbarushimana haingeweza kusababisha kubadilika kwa matokeo ya huu uchambuzi. Hii ni afere tofauti, yenye ililetwa mbele ya Chumba mpya, na yenye inahusu mtu tofauti na ambayo hali yenye kuhusu utoaji wa ushahuda haina kanuni kali.

<sup>19</sup> *Angalia pia* Chumba cha utangulizi II, “Decision on the Prosecutor’s Application for Summons to Appear for William Samoei Ruto, Henry Kiprono Kosgey and Joshua Arap Sang”, tarehe 8 mwezi wa tatu 2011, ICC-01/09-01/11-01, par. 12.

<sup>20</sup> Chumba cha rufaa, “Judgment on the appeal of the Prosecutor against the ‘Decision on the Prosecution’s Application for a Warrant of Arrest against Omar Hassan Ahmad Al Bashir”, ICC-02/05-01/09-73 (OA), par. 33, 39.

<sup>21</sup> Chumba cha utangulizi I, “Decision on the Confirmation of charges”, ICC-01/04-01/10-465.

<sup>22</sup> Chumba cha rufaa, “Judgment on the appeal of the Prosecutor against the decision of Pre-Trial Chamber I of 16 December 2011 entitled ‘Decision on the confirmation of charges’”, ICC-01/04-01/10-514 (OA 4).

21. Kwa hiyo, Chumba inapashwa kuchunguza ombi, maandiko yenye kuisindikiza na maelezo kwa ufupi ya ushahidi kutoka kwa Prokirere (« Alama ») ili kujua kama kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura alitenda jinai zenye anashtakiwa<sup>23</sup>.

#### A. Jinai dhidi ya ubinadamu

22. Bila kutoa hata moja, Chumba inaonesha kama maneno yenye inaandikwa ku artikle 7 ya Mkataba inaweza kuitwa jinai dhidi ya ubinadamu tuu, ikiwa kama ilitendwa katika hali ya shambulio yenye kupangwa na ya mkubwa, shambulio juu ya basivile na yenye ilipangwa kwa kujua. Kufuatana na artikle 7-2-a ya Mkataba, « kushambulia basivile», inamaanisha mwenendo ya kutenda matendo mara mingi kama vile inaandikwa ku artikle 7-1. Ni matendo yenye kuhusu basivile fulani. Na hiyo inatendwa kufuatana na siasa ya inchi ao ya shirika yenye kuwa na nia ya shambulio kama hilo. Inafaa kuonesha ya kwamba Inchi ao shirika fulani ilikuwa na siasa ya kufanya basivile bakuwe shabaha muhimu ya ile shambulio<sup>24</sup>. Alama za jinai zinaonesha wazi ya kwamba ili kusema kama kuna « siasa yenye mpango wa shambulio kama lile», inafaa inchi ao shirika fulani « isaidie ao iunge mkono shambulio kama ile juu ya basivile<sup>25</sup>».

23. Kufuatana na ushahidi yenye Prokirere alitoa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha ya kuamini kwamba: i) baFDLR banaweza kuitwa shirika kufuatana na artikle 7-2-a ya Mkataba, na ii) kwamba kati ya tarehe 20 mwezi ya kwanza 2009 na mwisho wa mwezi ya kenda 2010, baFDLR banabeba muzigo ya kutenda matendo mingi yenye inaandikwa ku artikle 7-1 ya Mkataba. Lakini, kwa kuona sababu zinazofuata, Chumba hakione ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba ile matendo ilitendwa kwa kutimiza ao kwa kufatisha siasa ya baFDLR yenye ina mpango wa kushambulia basivile.

<sup>23</sup> Chumba inarejea hapa tuu nusu ya alama zenye ilipokea na juu ya zenye ilitoa maamuzi yake ya jumla.

<sup>24</sup> *Angalia* Chumba cha Utangulizi II, "Decision Pursuant to Article 61(7)(a) and (b) of the Rome Statute on the Charges of the Prosecutor Against Jean-Pierre Bemba Gombo", ICC-01/05-01/08-424, par. 76.

<sup>25</sup> Artikle 7(3) ya Alama za jinai.

24. Kuhusu hali ya mpangilio ya baFDLR, ni kikundi yenye sisteme ya utawala wa msonge na yenye kuwa na mwenendo ya kuamua inayopangwa vizuri<sup>26</sup>. Matawi ya kisiasa na ya kijeshi zinaambatana sana<sup>27</sup>. Zilifanya pamoja kampanye ya kutangaza habari kwa mataifa juu ya kuunga mukono juhudi zabo za maswala ya kisiasa na kikijeshi<sup>28</sup>.

25. Kuhusu kiwango ya kushiriki ya baFDLR, amri ya kuunda « hali ya fujo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo<sup>29</sup> » kwa kuanzisha janga ya kibinadamu [*catastrophe humanitaire*] ilitolewa mwanzo wa mwaka 2009 chini ya mamulaka ya Sylvestre Mudacumura<sup>30</sup>. Tutazungumzia tena maneno ile katika kipindi ya kufuata. Katika muda yenye Prokirere aliangalia, basivile baliguswa na operesheni yenye baFDLR balifanya katika majimbo za Kivu<sup>31</sup>. Kati ya mwaka 2009 na mwaaka 2010, basivile baliuawa<sup>32</sup>, balitekwa nyara<sup>33</sup>, balibakwa,<sup>34</sup> balitendewa matendo ya ukatili<sup>35</sup> ao kukatwa viungo<sup>36</sup>, na

---

<sup>26</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 104, Uk. 10 na 22 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 59, par. 17 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 14 à 28 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 89, Uk. 10, 12, 24, 25, 54 na 55 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 56.

<sup>27</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 73, Uk. 14, 19 na 20 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 27, 83 na 84 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 77, Uk. 44 à 46.

<sup>28</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 644 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 43, Uk. 75.

<sup>29</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 19, Uk. 424 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 20, Uk. 171 à 173 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, Uk. 151 na 152.

<sup>30</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 426 na 427 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 30, Uk. 91, 94 na 122 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 84 à 90.

<sup>31</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 36 na 37 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 15 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 57, Uk. 11 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 79, Uk. 14 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 842 à 850 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 48, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 96, Uk. 5 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 69, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 42 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 65, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 97, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 123, Uk. 5 à 8 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 164 à 169, 175 à 179 na 187 à 190.

<sup>32</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 22, 25 à 28, 39 na 42 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 48, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 164 à 169.

<sup>33</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 19, Uk. 497 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 69, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 82.

<sup>34</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, Uk. 770 à 776 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 58, Uk. 5 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 69, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 175 à 179.

<sup>35</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, Uk. 775 na 776 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 48, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 39.

<sup>36</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 36 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 58, Uk. 5 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 82.

nyumba zabo zilibomolewa<sup>37</sup>. Operesheni za kijeshi za baFDLR ziliacha pia basivile banahama<sup>38</sup>.

26. Lakini, mashambulio yote yenye Prokirere anazungumuzia zilifanywa na baFDLR juu ya kulipisha kisasi fasi kulikuwa ba jeshi. Alama mingi zinaonesha pia ya kwamba baFDLR balikuwa na siasa ya kutosumbua basivile ao kubates<sup>39</sup> na kwamba bakubwa ya ile kundi habakuwa banapenda basivile bauwawe wakati ya ma operesheni<sup>40</sup>. Matukio yenye Prokirere anadai zilitokea sana sana wakati kidogo kiisha mashambulio kati ya jeshi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo [*Forces armées de la République démocratique du Congo (FARDC)*] na baFDLR katika eneo<sup>41</sup> ile ile moja. Hali hii inakuja kuhakikisha malipizi ya kisasi. Hata kama kuna mashambulio za kulipisha kisasi zilikuwa zinafanywa zikilenga vituo ya majeshi, pia na basivile benye habakuwa banapigana vita, hakuna namuna ya kusema ya kwamba inamaanisha wazi kama amri ya kuanza janga ya kibinadamu [*catastrophe humanitaire*] ilitendwa kabisa na majeshi ya FDLR katika eneo kwa kutimiza siasa yenye ilitiliwa na shirika na yenye ilivizia kushambulia basivile peke yake. Kutoheshimisha kanuni ya sheria ya kimataifa kuhusu binadamu haimaanishe peke yake kuwepo kwa siasa kama hiyo, tukizingatia hali ya mambo kama vile alama ya ushuhuda inaonyesha.

27. Kwa hiyo, Chumba inaona ya kwamba ushahidi yenye ililetwa haienee kwa kuamua kabisa sababu hizo ya kwamba operesheni za baFDLR zilikuwa katika hali ya kampanye kubwa ya kupangwa, hasa ya kushambulia basivile.

<sup>37</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 19, Uk. 497 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 22 na 25 à 28 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 801 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 49, Uk. 6 na 7 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 51, Uk. 3 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 187 na 188.

<sup>38</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 15 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 65, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 67, Uk. 3 à 8 na 71 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 72, Uk. 160 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 10 à 45 na 82 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 75, Uk. 29, 30 na 48 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 40 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 81, Uk. 16 à 37.

<sup>39</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 5, Uk. 10 na 11 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 7, Uk. 18 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 810 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 426 à 429, 433 na 434.

<sup>40</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 15, Uk. 180 na 181 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 16, Uk. 91 na 615 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 21, Uk. 813 à 815.

<sup>41</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 11, Uk. 45 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, Uk. 47 na 48 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, Uk. 229 à 231 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 20, Uk. 167 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 30, Uk. 76.

28. Chumba inakumbusha kama ku mwezi ya kenda 2010, Chumba cha utangulizi I iliamuaka ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kama, baFDLR kama vile shirika, baliundaka mwaka 2009 siasa yenye ilikuwa na lengo ya kushambulia basivile<sup>42</sup>. Lakini, kufuatana alama za hii dosye ya sasa (zenye ziliongezeka tangu mwezi ya kenda 2010), Chumba inaona ya kwamba wazo la kuwepo kwa siasa kwa ngazi ya shirika haiwezi kudaiwa.

29. Kufuatana na sababu zile, Chumba inaamua ya kwamba kutokana na kwamba hakuwepo siasa kwa ngazi ya shirika hilo, hakuna sababu za kutosha za kuamini kwamba baFDLR balitenda jinai dhidi ya ubinadamu kati ya tarehe 20 mwezi ya kwanza 2009 na mwisho ya mwezi ya kenda 2010.

## **B. Jinai za kivita**

### 1) Alama za hali za jinai ya kivita

30. Mbele ya kuchunguza alama zenye Prokiree alileta, Chumba itaangalia kwanza kama alama za hali za jinai zinaenea. Kama vile tutaiona, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba alama za hali za jinai za kivita zeye ziliandikwa katika Ombi zinaenea.

31. Chumba inaona ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba katika majimbo ya Kivu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kulikuwa vita kali kati ya majeshi ya serkali, ba FARDC, bakipigana benyewe ao bakiungana na majeshi ya Rwanda ao na majeshi ya *Mission de l'Organisation des Nations Unies en République démocratique du Congo* (MONUC ou MONUSCO), bakipigana na baFDLR, benye balikuwa bakipigana benyewe ao bakiungana na makundi zingine zenye silaha<sup>43</sup>. BaFDLR biko na muundo wa

<sup>42</sup> Chumba cha utangulizi I, "Decision on the Prosecutor's Application for a Warrant of Arrest against Callixte Mbarushimana", ICC-01/04-01/10-1, par. 26.

<sup>43</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 71, par. 3 à 13 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 73, Uk. 13 na 14 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 83, Uk. 12 na 15.

msonge wa chewe, banatii kamanda mkubwa na biko na uwezo ya kupanga na kuendesha operesheni ya kijeshi<sup>44</sup>.

32. Vita hii ilianza tarehe 20 mwezi wa kwanza 2009 wakati majeshi ya Rwanda *Forces rwandaises de défense* (FRD) iliingia katika eneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kujiunga na majeshi ya FARDC bakiendesha operesheni pamoja. Operesheni ile iliitwa « Umoja Wetu » na ilikuwa na nia ya kufukuza baFDLR ku ma kambi yabo ya Nord-Kivu na kusaidia waaskari ya FDLR benye bangelipenda kutoka ku jeshi na kurudi katika maisha ya kisivile mu Rwanda<sup>45</sup>. Mashambulio yenye ilifanyika na baFDLR kati ya mwezi wa kwanza na mwisho wa mwezi ya pili 2009, ilifanyika na majeshi yenye ilikuwa inapiganisha muungano ya majeshi ya FARDC na ya FRD<sup>46</sup>. Tarehe 25 mwezi ya pili 2009, majeshi ya FRD ilianza kuondoka Nord-Kivu<sup>47</sup> na majeshi ya FARDC ikaanza, ikisaidiwa na majeshi ya MONUC, operesheni *Kimia II*. Ilikuwa operesheni ya kijeshi ya kufuatilia hali ya mambo katika majimbo ya Nord-Kivu na Sud-Kivu. Nia yake ilikua kumaliza nguvu zote za baFDLR chini na kubazuia kurudiana pozisheni zabo za zamani na kufanya basipate mapato kwenye balikua bayapata<sup>48</sup>. Kufuatana na operesheni *Kimia II*, baFDLR balishambulia basivile kwa kulipiza kisasi na pia bakashambulia pozisheni za FARDC<sup>49</sup> ilikuwa inapatikana. Operesheni *Kimia II* ilianza tarehe 2 mwezi ya tatu 2009 na iliendelea mpaka tarehe 31 mwezi ya kumi na mbili 2009<sup>50</sup>.

33. Kiisha operesheni *Kimia II* kumalizika tarehe 31 mwezi ya kumi na mbili 2009, operesheni ya kijeshi ya pamoja kati ya ba FARDC na MONUC, operesheni *Amani Leo*,

<sup>44</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 59, par. 17; Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 14 à 28; Ombi ya Prokirere, nyongeza 89, Uk. 10, 12, 24, 25, 54 na 55; Ombi ya Prokirere, nyongeza 104, Uk. 10 na 22; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 56.

<sup>45</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 9, Uk. 27; Ombi ya Prokirere, nyongeza 50, Uk. 3 na 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 64, Uk. 3; Ombi ya Prokirere, nyongeza 73, Uk. 7 na 13; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 8; Ombi ya Prokirere, nyongeza 83, Uk. 12.

<sup>46</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 50, Uk. 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 64, Uk. 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 8.

<sup>47</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 50, Uk. 4.

<sup>48</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 19, Uk. 323 à 326; Ombi ya Prokirere, nyongeza 50, Uk. 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 51, Uk. 2 à 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 52, Uk. 3.

<sup>49</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 52, Uk. 3; Ombi ya Prokirere, nyongeza 73, Uk. 14; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, Uk. 9.

<sup>50</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 51, Uk. 2 na 3; Ombi ya Prokirere, nyongeza 53, Uk. 3; Ombi ya Prokirere, nyongeza 64, Uk. 4; Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, Uk. 51.

ilianza juu ya kupiganisha baFDLR ku mwezi ya kwanza 2010. Lengo yake ilikuwa kukinga basivile, kuzuia baFDLR na makundi ingine yenye silaha kutoshambulia na kutolipiza kisasi katika majimbo ya Nord-Kivu na Sud-Kivu, pia muungano ya majeshi ipate kukamata na kutawala ile eneo na eneo za mhimu kwenye baFDLR balifukuzwaka<sup>51</sup>. BaFDLR baliendelea kulipiza kisasi bakijiunga na makundi mengine yenye silaha na kuingia katika vijiji ndogo ndogo<sup>52</sup>. Hata kama ba FARDC mu mwezi ya kwanza 2010 balifanya operesheni ya kijeshi bao benyewe, lakini tarehe 26 mwezi ya pili 2010, mu majimbo ya Kivu, balizifanya bakazipanga na MONUC na bakasaidiwa na MONUSCO katika ile iliitwa operesheni *Amani Leo*<sup>53</sup>, operesheni zenye ziliendelea juu ya mashambulio yenye shabaha<sup>54</sup>. Ripoti zinaonesha ya kwamba katikati ya mwaka 2010, basoda 60000 ya FARDC na batalioni [*bataillons*] kumi ya kulinda amani ya MONUC zilitumiwa mu majimbo ya Kivu<sup>55</sup>, wakati baFDLR balikuwa banaendelea kushambulia kwa kulipisha kisasi<sup>56</sup>.

34. Kufuatana na ushahidi yenye ilitolewa, Chumba inaona ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba: i) tangu tarehe 20 mwezi ya kwanza 2009 mpaka tarehe 25 mwezi ya pili 2009, tangu tarehe 2 mwezi ya tatu 2009 mpaka tarehe 31 mwezi ya kumi na mbili 2009, na tangu mwezi ya kwanza 2010 mpaka mwisho wa mwezi ya kenda 2010, majimbo ya Kivu katika eneo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zilikuwa fasi ya vita kali, kwa muda murefu, na haikukuwa vita ya aina ya kimataifa kufuatana na artikle 8-2-f ya Mkataba ; ii) vita ile ilikuwa kati ya baFDLR, benye balikuwa saa moja bakijiunga na makundi mengine, na ba FARDC, bakijiunga na ba FDR wakati ya operesheni *Umoja Wetu* na bakijiunga na MONUC wakati ya operesheni *Kimia II* na *Amani Leo* ; na iii) baFDLR ni kundi yenye silaha na yenye mpangilio kufuatana na artikle 8-2-f ya Mkataba. Kwa hiyo Chumba inaamua ya kwamba matendo ya jinai yenye baFDLR banashtakiwa, kama vile

<sup>51</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 35 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 53, Uk. 16 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 71, Uk. 3 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 14 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 83, Uk. 12.

<sup>52</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 14.

<sup>53</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 71, Uk. 3.

<sup>54</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 71, Uk. 3.

<sup>55</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 83, Uk. 12.

<sup>56</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 65, Uk. 2 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 76, Uk. 14 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 83, Uk. 15.

zilichunguzwa hapa chini, zilitendwa katika hali ya vita isiyokuwa ya kimataifa na balishiriki kwenye ile vita.

2) Matendo yenye kuunda jinai zenye zilitendwa katika hali ya vita isiyokuwa ya kimataifa ao zilizotendwa kwa uhusiano na hali hii

35. Prokirere anataja mashtaka kenda kuhusu jinai za kivita. Chumba itachunguza matendo yenye inatajwa ndani ya Ombi ya Prokirere juu ya kuhakikisha kama kuna sababu za kuamini kwamba jinai za kivita zilitendwa kufatana na artikle 8 ya Mkataba.

*Jinai ya kivita ya shambulio dhidi ya basivile (artikle 8-2-e-i ya Mkataba, shtaka 1)*

36. Ku shtaka 1, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya kutenda jinai **kwa kushambulia kwa makusudi basivile** katika mahali mbalimbali ya majimbo ya Nord-Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kandokando ya pale, sawa vile pale **Kipopo**, katika mtaa [*territoire*] wa Masisi, katika Nord-Kivu tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao karibu ya zile tarehe; pale **Mianga**, katika mtaa [*territoire*] wa Walikale, katika Nord-Kivu tarehe 12 mwezi ya ine 2009 karibu ya ile tarehe; pale **Busurungi** na katika vijiji ya kandokando, katika mtaa [*territoire*] ya Walikale, katika Nord-Kivu tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibu ya zile tarehe; pale **Manje**, katika mtaa [*territoire*] wa Masisi, katika Nord-Kivu tarehe 20 na 21 mwezi ya saba ao karibu ya zile tarehe; pale **Malembe**, katika mtaa [*territoire*] wa Walikale, katika Nord-Kivu mwisho wa mwezi ya saba na mwanzo ya mwezi ya katikanane, na tangu tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi ya munane, ma pia tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao karibu ya zile tarehe; [IMEVUTWA]<sup>57</sup>.

37. Kutokana na ushahidi yote yenye ilioneshwa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba basivile balishambuliwa na baFDLR, kufuatana na artikle 8-2-e-i ya Mkataba : i) pale Kipopo tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao karibia zile tarehe<sup>58</sup>, ii) pale Mianga tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao karibia ile tarehe<sup>59</sup>, iii) pale Busurungi na mu vijiji ya kandokando tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibia zile tarehe<sup>60</sup>, iv) pale Manje tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibia zile tarehe<sup>61</sup>, v) pale

<sup>57</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31.

<sup>58</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, Uk. 206 à 215 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 454 à 457 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 16 à 18 na 20.

<sup>59</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 440, 442 na 443 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, Uk. 215 na 216 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 57, Uk. 4, 7 na 13.

<sup>60</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 11, Uk. 45 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 12, Uk. 221, 229 na 267 à 284.

<sup>61</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 458 à 460 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, Uk. 474 à 491.



Malembe mwisho wa mwezi ya saba 2009<sup>62</sup>, mwanzo wa mwezi ya munane 2009<sup>63</sup>, tangu tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi ya munane 2009<sup>64</sup>, na tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao karibia ile tarehe<sup>65</sup>, [IMEVUTWA]<sup>66</sup>, [IMEVUTWA]<sup>67</sup>, [IMEVUTWA]<sup>68</sup>, na [IMEVUTWA]<sup>69</sup>.

38. Chumba inatia mkazo ikisema ya kwamba mashambulio zile zilikuwa zinalenga bila ubaguzi pozisheni ya basivile na ya bajeshi. Mashambulio ile iko chini ya artikle 8-2-e-i ya Mkataba, kwa kuona ya kwamba jinai ya kivita ya kushambulia basivile « haimainishe kama basivile tuu njo balikuwa sana sana shabaha ya mashambulio<sup>70</sup> ». Lakini, Chumba inaona ya kwamba mashambulio bila ubaguzi ni ya kutofautisha na mashambulio ya basivile kufuatana na artikle 7 ya Mkataba, mashambulio yenye basivile njo shabaha.

*Jinai za kivita za mauaji (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 2)*

39. Ku shtaka 2, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo wa kutenda jinai ya mauaji kama vile jinai za kivita, zenye zilitendwa na baFDLR ku basivile ba mahali mbalimbali za majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kandokando ya zile mahali, kama vile pale **Kipopo**, katika mtaa [territoire] wa Masisi, katika Nord-Kivu tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao karibu ya zile tarehe; pale **Busurungi**, katika mtaa [territoire] wa Walikale, katika Nord-Kivu tarehe 3 mwezi ya tatu 2009 ao karibu ya ile tarehe; pale **Mianga**, ku mtaa [territoire] wa Walikale, katika Nord-Kivu tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao karibu ya ile tarehe; pale **Busurungi** na katika vijiji ya kandokando tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibia zile tarehe; pale **Manje**, katika mtaa [territoire] wa Masisi, katika Nord-Kivu tarehe 20 na tarehe 21 mwezi ya saba na ao karibu ya zile tarehe; pale **Malembe**, katika mtaa [territoire] wa Walikale, katika Nord-Kivu tangu tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi ya munane, na tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao karibu ya zile tarehe; [IMEVUTWA]; pale **Mutakato**, katika mtaa [territoire] wa Walikale, katika Nord-Kivu tarehe 2 na 3 mwezi ya kumi na mbili 2009 ao karibu ya zile tarehe; [IMEVUTWA]<sup>71</sup>.

40. Kutokana na alama zote zenye zilioneshwa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kuamini kwamba jinai ya mauaji, kufuatana na artikle 8-2-c-i ya Mkataba

<sup>62</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 7 na 8.

<sup>63</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 8 à 10.

<sup>64</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, Uk. 186 à 188 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 10 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 56, Uk. 4 na 5 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 122, Uk. 7.

<sup>65</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 11 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 56, Uk. 5.

<sup>66</sup> [IMEVUTWA].

<sup>67</sup> [IMEVUTWA].

<sup>68</sup> [IMEVUTWA].

<sup>69</sup> [IMEVUTWA].

<sup>70</sup> Chumba cha utangulizi I, "Decision on the confirmation of charges", ICC-01/04-01/10-465-Red, par. 218.

<sup>71</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31.

ilitendwa na baFDLR juu ya sivile moja ao basivile mingi benye habakuwa banapigana vita: i) pale Kipopo tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao karibia zile tarehe<sup>72</sup>, ii) pale Busurungi tarehe 3 mwezi ya tatu 2009 ao karibia ile tarehe<sup>73</sup> na tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibia zile tarehe<sup>74</sup>, iii) pale Mianga tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao karibia ile tarehe<sup>75</sup>, iv) pale Manje tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibia zile tarehe<sup>76</sup>, v) pale Malembe kati ya tarehe 11 na tarehe 13 mwezi ya munane 2009<sup>77</sup>, na kwamba tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao karibia ile tarehe<sup>78</sup>, [IMEVUTWA]<sup>79</sup>, na [IMEVUTWA]<sup>80</sup>.

41. Kuhusu mambo yenye, kama Prokirere anasema, inawaziwa kuwa ilitendwa Mutakato tarehe 2 mwezi ya kumi na mbili 2009 ao karibia ile tarehe, Chumba inaona ya kama ushahidi yenye ilitolewa kuhusu yale mambo, ni ushahidi ya kwamba basivile balikimbiaka na bajeshi tuu njo baliuawa<sup>81</sup>. Pia, ripoti ya Umoja wa mataifa ilionesha ya kwamba “batu” bawili baliuwawa<sup>82</sup>. Kwa hiyo Chumba inaona ya kwamba ushahidi yenye ililetwa kwa kuunga mkono ile mashtaka hazitoshe kwa kuamua ya kwamba kuna sababu za kutosha kwa kuamini kwamba batu benye baliuwawa habakukuwa banashiriki kwenye vita ao balikuwa basivile ao bafanyakazi ya afya ao batumishi ya Mungu benye habakuwa banapigana vita kabisa.

*Jinai ya kivita ya kukata viungo vya mwili (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 4)*

42. Ku shtaka 4, Prokirere anadai hivi :

<sup>72</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 454 à 457 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 42, Uk. 16, 17 na 20.

<sup>73</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 23, Uk. 7 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 24, Uk. 5 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 31, Uk. 6.

<sup>74</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 12, Uk. 266 à 268 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 711, 712, 717 na 718 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 34, Uk. 5 na 6.

<sup>75</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 16, Uk. 483 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 32, Uk. 8 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 54, Uk. 7.

<sup>76</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 459 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 33, par. 31 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 188, Uk. 73.

<sup>77</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 10 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 56, Uk. 4 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 122, Uk. 7.

<sup>78</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, Uk. 11 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 56, Uk. 5.

<sup>79</sup> [IMEVUTWA].

<sup>80</sup> [IMEVUTWA].

<sup>81</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, Uk. 264.

<sup>82</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 55, Uk. 3 à 5.

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya jinai ya **kukata viungo ya mwili ya watu**, kama vile jinai ya kivita, tendo yenye ilifanywa na baFDLR pale **Busurungi** ao kandokando ya pale na ku vijiji ya kandokando, katika mtaa [territoire] wa Walikale, ku Nord-Kivu tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibu ya zile tarehe<sup>83</sup>.

43. Kutokana na ushahidi yote yenye ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba kukata viungo ya batu, kufuatana na artikle 8-2-c-i ya Mkataba ilitendeka, pale Busurungi tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao kandokando na zile tarehe: bajeshi baFDLR balitobola, bakitumia kisu ya bajeshi "*baïonnette*", macho ya bibi mweye alikuwa na mimba na luteni moja wa baFDLR alikata viungo ya buchi ya ba sivile ao wakatii ya vita katika hali ya kushambulia kwa kubalipisha ba FARDC<sup>84</sup> kisasi.

*Jinai za kivita za utendeaji wa kikatili (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 6)*

44. Ku shtaka 6, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya **matendo ya kinyama**, kama vile jinai ya kivita, zenye zilitendwa na baFDLR kwa kushambulia, bakiuimiza na/ao bakikaza basivile kubeba mizigo mizito ya bitu balipora. Hali ile ilileta maumivu ya nguvu na mateso ao hasara kubwa kwa mwili ao ya afya ya kimwili ao ya kiakili. Ile yote ilitendwa mahali mbalimbali katika majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kandokando ya zile majimbo, kama vile pale **Busurungi** na katika majimbo ya kandokando, mtaa [territoire] wa Walikale, mu Nord-Kivu tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibia zile tarehe; pale **Manje**, mtaa [territoire] wa Masisi, ku Nord-Kivu tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibia zile tarehe ; [IMEVUTWA]<sup>85</sup>.

45. Kufuatana na ushahidi yote ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba matendo ya ukatili kufuatana na artikle 8-2-c-i ya Mkataba zilitendwa : i) pale Busurungi na katika vijiji jirani tarehe 9 na 10 mei 2009 ao karibu ya zile tarehe, wakati [IMEVUTWA]<sup>86</sup>, ii) pale Manje tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibu ya zile tarehe, wakati [IMEVUTWA]<sup>87</sup>, [IMEVUTWA]<sup>88</sup>, [IMEVUTWA]<sup>89</sup>.

<sup>83</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31.

<sup>84</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, Uk. 412 à 414 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, Uk. 333, 751 na 752 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 34, Uk. 5.

<sup>85</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza par. 31.

<sup>86</sup> [IMEVUTWA].

<sup>87</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 33, uk. 5 mpaka 10.

<sup>88</sup> [IMEVUTWA].

<sup>89</sup> [IMEVUTWA].

*Jinai za kivita za ubakaji (artikle 8-2-e-vi ya Mkataba, shtaka ya 7)*

46. Ku shtaka 7, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya ubakaji, kama vile jinai ya kivita, ilitendwa na ba soda yake ya FDLR dhidi ya basivile sehemu mbali mbali katika majimbo za Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kandokando yake. Kwa mufano, **Busurungi** na kwenye vijiji jirani kwenye mkoa wa Walikale, ku Nord-Kivu. Ilikuwa mwisho wa mwezi ya ine ao ku mwanzo wa mwezi ya tano na tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibu ya zile tarehe ; [IMEVUTWA] ; **Manje** huko Masisi, mu Nord-Kivu tangu tarehe 20 na tarehe 21 mwezi ya saba 2009 ao karibu ya zile tarehe ; [IMEVUTWA]<sup>90</sup>

47. Kufuatana na ushahidi yenye ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba jinai ya ubakaji kufuatana na artikle 8-2-e-vi ya Mkataba, ilitendwa, basoda ya FDLR balishika mwili ya mtu moja wakamuingiza mbolo kwa nguvu ao kwa kutumia nguvu, na pale : i) Busurungi na katika vijiji jirani tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao karibu ya zile tarehe<sup>91</sup>, [IMEVUTWA]<sup>92</sup>, iii) pale Manje tarehe 20 mpaka tarehe 21 mwezi ya saba 2009 ao karibu ya zile tarehe<sup>93</sup>, [IMEVUTWA]<sup>94</sup> na [IMEVUTWA]<sup>95</sup>.

48. Chumba inaona kama Prokirere ana taja matendo ilitendeka pale Busurungi « [TAFSIRI] kwa mwisho ya mwezi ya ine ao ku mwanzo ya mwezi ya tano[2009] » bila kupana mafasiriyo katika ombi yake ao kuleta ufupi ya ushahidi ya kuonesha matendo yale. Chumba inaona ya kwamba hakuna zababu za kutosha za kuamini kwamba jinai ya ubakaji ilitendeka pale Busurungi kwa mwisho ya mwezi ya ine ao mwanzo ya mwezi ya tano 2009.

*Jinai za kivita za mateso (Artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 9)*

49. Ku shtaka 9, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya jinai ya kutesa, kama vile jinai ya kivita, yenye ilitendeka kwa njia ya kutesa watu vikali sana, kwa njia ya ubakaji ya nguvu kabisa, kwa njia ya kuumiza na/ao matendo ya kinyama waliofanyia wa viktime na ikabaleta maumivu namateso magumu sana, ya

<sup>90</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31.

<sup>91</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 24, uk. 8 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 25, uk. 8 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 34, uk. 5

<sup>92</sup> [IMEVUTWA].

<sup>93</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 118, uk. 73 na 74.

<sup>94</sup> [IMEVUTWA].

<sup>95</sup> [IMEVUTWA].

kimwili ao ya kiakili. Walitaka watisha, kuwapatia malipizi ao kuwatendea ubaguzi kufuatana na ginsi waliunga mukono FARDC. Hayo yalitendeka sehemu nyingi katika majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kando kando yake. Busurungi na kwenye ma vijiji jirani, katika eneo ya Walikale, ao ku Nord-Kivu tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao kwa zile tarehe; [IMEVUTWA]<sup>96</sup>.

50. Kufuatana na ushahidi yote iliyoletwa, Chumba inaamua ya kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba mateso, kama vile inafasiriwa mu artikle 8-2-c-i ya Mkataba, ilitendwa na basoda ya FDLR benye balitesa kabisa kimwili na kiakili basivile mingi kama kuwapa malipizi. Na hii ilifanyika Busurungi na ku vijiji jirani tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe, wakati basivile balipigwa na kubakwa, kukatwa viungo ya mwili na kuwatendewa matendo ya kinyama na basoda ya baFDLR. Ilikuwa namna ya kuwapa malipizi kwa madai ya kuunga mkono FARDC<sup>97</sup>, [IMEVUTWA]<sup>98</sup>, na [IMEVUTWA]<sup>99</sup>.

*Jinai za kivita za kubomoa vitu (artikle 8-2-e-xii ya Mkataba, shtaka 11)*

51. Ku shtaka 11, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya jinai ya **kubomoa bitu ya adui** ao kuharibu mali yenye haihusu mahitaji ya kijeshi na matendo yenye ilitendwa sana. Hii ni jinai ya kivita yenye ilitendwa na baFDLR, benye balichoma kwa jumla nyumba na majengo ya basivile sehemu mbalimbali za majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kando kando, kama pale Kipopo, huko Nord-Kivu tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe ; pale **Mianga**, mtaa wa Walikale ku Nord-Kivu tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao Nord-Kivu ile tarehe ; pale **Busurungi** na kwenye vijiji jirani katika mtaa wa Masisi, Nord-kivu tarehe 9 na tarehe 10 mwezi ya tano 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe ; pale **Manje** katika mtaa ya Masisi, Nord-Kivu tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe; **Malembe**, katika mtaa wa Walikale, ku Nord-Kivu pale mwanzo wa mwezi ya nane, tangu tarehe 11 mpaka 13 mwezi ya nane na tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe, [IMEVUTWA].<sup>100</sup>

52. Kufuatana na ushahidi yote yenye ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kama matendo ya kuharibu mali, namna inaandikwa kwa artikle 8-2-e-xii ya Mkataba, kama ilitendwa na basoda ya FDLR benye baliharibu ao balinyanganya bitu yenye haikukua lazma kwa matumizi ya kijeshi. Mali ya adui yenye inapashwa kulindwa kufuatana na sheria ka kimataifa yenye inahusu vita, na hii ilifanyika i) pale Kipopo tarehe 12 na 13 mwezi ya pili 2009 ao, Nord-Kivu zile tarehe,

<sup>96</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31.

<sup>97</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 25, uk. 4 na 6 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 31, uk. 4 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, uk. 752.

<sup>98</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 28, uk. 6 na 7 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 29, uk. 5 na 6 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 38, uk. 6.

<sup>99</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 26, uk.9 na 10; Ombi ya Prokirere, nyongeza 61, uk. 1 mpaka 8, Ombi ya Prokirere, nyongeza 61, uk 1 mpaka 8, Ombi ya Prokirere, nyongeza 70, uk. 14.

<sup>100</sup> Ombi ya Prokirere, par. 31

wakati baFDLR balilunguza nyumba mingi za vijiji wakati ya shambulio yenye ililenga pia pozisheni ya basoda ya FARDC<sup>101</sup>, ii) pale Mianga tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao Nord-Kivu ile tarehe wakati baFDLR balichoma nyumba za basivile wakati wa shambulio yenye kupata ushindi na kisha ile shambulio yenye ililenga pozisheni ya basoda ya FARDC<sup>102</sup> iii) pale Busurungi na katika vijiji jirani tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe, wakati nyumba mingi za basivile zilichomwa wakati na nyuma ya vita na ba FARDC<sup>103</sup> iv) pale Manje tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe, wakati nyumba za basivile zilichomwa na baFDLR ya kukimbia ya ba FARDC kutoka ile kijiji<sup>104</sup> ; v) pale Malembe ku mwanzo ya mwezi ya munane 2009<sup>105</sup>, tangu tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi ya munane 2009<sup>106</sup>, na tarehe 15 mwezi ya kenda 2009<sup>107</sup>, ao karibia ile tarehe wakati baFDLR balichoma nyumba ya basivile mara mingi, [IMEVUTWA]<sup>108</sup>, [IMEVUTWA]<sup>109</sup>, na [IMEVUTWA]<sup>110</sup>

*Jinai za kivita za uporaji (Artikle 8-2-e-v ya Mkataba, shtaka 12)*

53. Ku shtaka 12, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya jinai ya **uporaji** ya mali ya basivile, hii ni jinai ya kivita. Ni mali kama vile franka, zahabu, vifaa ya nyumbani, chakula na mifugo zenye zilichukulia sehemu mbali mbali katika majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ao kando kando, kama vile **Mianga**, mtaa wa Walikalie ku Nord-Kivu tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao Nord-Kivu ile tarehe ; pale **Busurungi** na katika vijiji jirani ya mtaa ya Walikale ku Nord-Kivu, tarehe 9 na 10 mwezi ya tano 2009 ao Nord-Kivu zile tarehe ; pale **Manje**, mtaa ya Masisi, Nord-Kivu tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibia zile tarehe ; pale **Malembe** ku eneo ya Walikale, ku Nord-Kivu ku mwisho ya mwezi ya saba 2009, tangu 11 mpaka 13 mwezi ya munane na tarehe 15 mwezi ya kenda na tarehe 15 mwezi ya kenda 2009 ao karibia zile tarehe, [IMEVUTWA]; pale **Mutakato** ku

<sup>101</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, uk. 212 na 213 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, uk. 454 na 455 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 30, uk. 152 mpaka 155, Ombi ya Prokirere, nyongeza 57, uk. 11.

<sup>102</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 20, uk. 174 mpaka 176 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, uk. 215 na 216 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, uk. 83.

<sup>103</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, uk. 53 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, uk. 428 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 23, uk. 11 na 13.

<sup>104</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, uk. 483 na 484 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 33, uk. 6 na 9 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 74, uk. 83.

<sup>105</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, uk. 8 mpaka 10

<sup>106</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 13, uk 130 na 131 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, uk 392 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, uk. 10, Ombi ya Prokirere, nyongeza 122, uk. 7.

<sup>107</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, uk.11.

<sup>108</sup> [IMEVUTWA].

<sup>109</sup> [IMEVUTWA].

<sup>110</sup> [IMEVUTWA].

mtaa ya Walikale huko Nord-Kivu tarehe 2 na 3 mwezi ya kumi na mbili 2009 ao karibia zile tarehe ;  
[IMEVUTWA]<sup>111</sup>

54. Kufuatana na ushahidi yote yenye ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kama matendo yenye kuunda jinai ya uporaji kama vile inaandikwa kwa artikle 8-2-e-v ya Mkataba ilitendeka na basoda ya FDLR benye balijipatia mali ya batu bila ruhusa ili babitumiye, i) jambo ile ilifanyika pale Mianga tarehe 12 mwezi ya ine 2009 ao karibia ile tarehe wakati baFDLR balikuwa banatafuta chakula na manguo, balichukua mali ya basivile<sup>112</sup> ii) Busurungi na katika vijiji jirani tarehe 9 na 10 mei 2009 ao karibia zile tarehe. Wakati wa ile shambulio, baFDLR balichukua mifugo, nguo na bitu vifaa ingine ya munyumba ya basivile<sup>113</sup> iii) pale Manje tarehe 20 na 21 mwezi ya saba 2009 ao karibia zile tarehe, baFDLR balichukua chakula ya basivile na pia bitu bingine ya munyumba<sup>114</sup>, iv) pale Malembe mwisho ya mwezi ya saba 2009<sup>115</sup> na tangu tarehe 11 mpaka tarehe 13 mwezi ya munane 2009<sup>116</sup>, nyumba za basivile ziliporwa mara mingi, [IMEVUTWA]<sup>117</sup>, vi) pale Mutakato tarehe 2 na 3 mwezi ya kumi na mbili 2009 ao karibia zile tarehe, wakati mali ya basivile hata na mifugo bilichukuliwa na baFDLR<sup>118</sup>, [IMEVUTWA]<sup>119</sup>, na [IMEVUTWA]<sup>120</sup>.

*Jinai za kivita za kuvunja batu heshima (artikle 8-2-c-ii ya Mkataba, shtaka 14)*

55. Ku shtaka 14, Prokirere anadai hivi :

[TAFSIRI] Sylvestre MUDACUMURA anabeba muzigo ya jinai ya kukosea heshima batu, kama vile jinai ya kivita, iliyofanyika nafasi mbali mbali katika majimbo ya Kivu (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), kama vile [IMEVUTWA]<sup>121</sup>.

<sup>111</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 31

<sup>112</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 16, uk. 483 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, uk. 242

<sup>113</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 17, uk. 396, 397, 754 na 755 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 18, uk 263 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 54, uk. 6.

<sup>114</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 33, uk.8.

<sup>115</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, uk. 7 na 8

<sup>116</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 37, uk. 10; Ombi ya Prokirere, nyongeza, nyongeza 122, uk. 7.

<sup>117</sup> [IMEVUTWA].

<sup>118</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 39, uk. 264; Ombi ya Prokirere, nyongeza 55, uk. 4.

<sup>119</sup> [IMEVUTWA].

<sup>120</sup> [IMEVUTWA].

<sup>121</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 31.

56. Kufuatana na ushahidi yote yenye ilitolewa, Chumba inaamua ya kwamba kuko sababu zakutosha za kuamini kwamba matendo ya kukosea heshima batu, kama vile inaandikwa katika artikle 8-2-c-ii ya Mkataba, zilitendwa na basoda ya FDLR benye balifanyia sivile moja ao basivile mingi matendo ya kazarau na ya kushusha heshima ao matendo yenye ilituma sifa yabo izarauliwe. Uzito wa Matendo yale niyakuchukulia kwa jumla kama ya kukosesha batu heshima. [IMEVUTWA]<sup>122</sup>.

3) Kwa kumaliza

57. Kufuatana na yote ya mbele, Chumba inaona ye kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba matendo yenye inaunda jinai zenye zilitajwa zilitendwa. Kama vile tuliona hapa juu, ilikuwa katika hali vita yenye ilifanyika mu majimbo za Kivu na mambo yenye kuambatana na vita ile. Mashambulio ya basivile, mauaji, kukata viungo ya mwili, matendo ya kinyama, ubakaji, kutesa, kuharibu vitu, uporaji, kukosea watu heshima, yote ilikuwa ikiambatana na vita ile, kwa sababu makosa yale ya jinai ilitendwa juu ya ile vita.

58. Kufuatana na ushahidi yote yenye ilitolewa, Chumba inaamua pia ya kwamba kuna sababu za kutosha za kuamini kwamba benye balitenda zile jinai balikuwa kweli na nia mbaya ya kutenda jinai zinazotajwa hapa juu, kama vile *ulterior intent* yenye inahitajika ili kuwe jinai hizo. Kwa hiyo, Chumba inaamua ya kwamba baFDLR balitenda jinai za kivita hizi : shambulio ya basivile, mauaji, kukata watu viungo ya mwili, matendo ya kinyama, kubaka, mateso, kuharibu mali, kupora, kukosea watu heshima, hizi zote zinatolewa malipizi kufuatana na artikle 8-2-c-i, 8-2-c-ii, 8-2-e-i, 8-2-c-ii, 8-2-c-ii, 8-2-e-v, 8-2-e-xii ya Mkataba.

---

<sup>122</sup> [IMEVUTWA].



III. Kweli, kuna sababu zakutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anabeba muzigo ya jinai zenye kupatikana katika ombi ya Prokirere ?

59. Mu sehemu ya Ombi mwenye muko mashtaka, Prokirere anapendekeza aina tatu za uwezekano wa kubebesha Sylvestre Mudacumura kibinafsi mzigo wa jinai: i) kutenda pamoja na batu bengine bila kuwa moja kwa moja kama vile inaandikwa katika artikle 25-3-a, ii) kuamuru batu kutenda jinai, kama vile inaandikwa katika artikle 25-3-b ya Mkataba, na iii) kubeba muzigo kama mukubwa wa ngazi zote kama vile inaandikwa katika artikle 28-a ya Mkataba<sup>123</sup>.

60. Kuhusu aina ya kwanza ya kubeba muzigo ya jinai yenye inaletwa katika ombi ya Prokirere, ikiwa ni kutenda pamoja na batu bengine isiyokuwa ya moja kwa moja, Chumba inakumbusha kama ile aina ya muzigo ya jinai inabidi mtu yule ahuzurie katika mupango ya pamoja ao kuwa alikubaliana na alama moja kati ya zenye kuunda jinai<sup>124</sup>.

61. Chumba inaonesha kama kuhusu mupango ya pamoja ya FDLR, Prokirere alisema kama viongozi ya kisiasa na ya kijeshi ya kikundi hiki ilikubali kuanzisha, na kikafanya mashambulio kubwa na yenye kupangwa dhidi ya basivile ndani ya majimbo za Kivu, na pia kikatumia vyombo vya habari kusudi ya kutafuta FDLR ipate madaraka kuinguvu kule Rwanda<sup>125</sup>

62. Kwa hivi, Chumba inatiya mukazo ya kwamba hizi jambo ya mupango ya pamoja na ya siasa yenye kuwa na lengo ya kutenda jinai dhidi ya ubinadamu inaambatana hata kama haiko kitu moja. Kwa kuwa Chumba ilifikia uamzi ya kwamba FDLR haikukuwa na siasa ya kuongoza kweli mashambulio dhidi ya basivile kama vile basivile<sup>126</sup>, Chumba inaona kama Prokirere naye hakuonesha sababu za kutosha za kuamini kama mupango

<sup>123</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 31

<sup>124</sup> Chumba cha utangulizi II, *Decision on the Confirmation of charges pursuant to Article 61(7)(a) and (b) of the Rome Statute*, ICC-01/09-01/11-373, par. 301, 305, 313 et 333; Chumba cha utangulizi II, *“Decision on the Confirmation of Charges Pursuant to Article 61(7)(a) and (b) of the Rome Statute”*, ICC-01/09-02/11-382-Red, par. 297 ; Chumba cha utangulizi I, *“Decision on the confirmation of charges”*, ICC-01/04-01/07-717, par. 500-14, 527-39.

<sup>125</sup> Ombi ya Prokirere, nyongeza 70.

<sup>126</sup> Ona juu, nukta 22 mpaka 29.

ya pamoja yenye anasema ilioneshwa, kufuatana na ginsi katika ombi yake alifanya uhusiano kati ya hii mambo mbili mbali mbali. Kwa upekee, hakuna kitu inaonesha kama uongozi ya siasa na ya kijeshi ya FDLR ilifanya mbele au nyuma makubaliano au balisikilizana kuhusu mupango ya pamoja yakufanya basivile kuwa lengo kubwa ya mashambulio yao. Zaidi ya pale, ushahidi yenye ilioneshwa haitoshe kwa kuonesha kama amri ya kuanza janga ya kibinadamu mu majimbo za Kivu ilitokana na mazungumuzo au makubaliano, ili ionekane kama kulikuwa na mpango ya pamoja kutoka kwa viongozi wa kisiasa na kijeshi wa FDLR.

Kufuatana na hii maneno, Chumba inaamua ya kwamba hakuna sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anabeba muzigo ya jinai kama vile mtendaji isiyekuwa wa moja kwa moja, kama vile inaandikwa mu artikle 25-3-a ya Mkataba, wa jinai za kivita zenye zimetajwa hapa juu.

63. Kuhusu aina ya pili ya kubeba muzigo ya jinai yenye Prokirere alisema, Chumba inakumbusha kama, kufuatana na artikle 25-3-b ya Mkataba, hapa ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, tendo ya kuamuru jinai itendeke ni aina moja ya kubeba muzigo ya jinai kama vile mtendaji mshiriki (*complice*)<sup>127</sup>. Iki kubaliana na namna Mahakama za kimataifa za jinai za muda zilifasiria neno kubeba muzigo ya jinai kutokana na amri yenye mtu alipana<sup>128</sup>, Chumba inaona ya kwamba, kufuatana na artikle 25-3-b ya Mkataba, ili mtu aonekane kama vile anabeba muzigo ya jinai, inapashwa kuonyeshwa kama : a) mtu yule alikuwa na cheo na mamlaka<sup>129</sup>, b) kama mtu huyu alitoa amri kwa njia yeyote kwa mtu mwingine<sup>130</sup>, kwa nia ya i) kutenda jinai, wakati ile jinai ilifanyika wala ilijaribu

<sup>127</sup> Chumba cha utangulizi I, "Decision on the Confirmation of Charges", ICC-01/04-01/07, par. 517 ; Chumba cha utangulizi I, *Décision sur la confirmation des charges*, ICC-01/04-01/06-803, par. 320 na 321.

<sup>128</sup> *Ona*, artikle 21-1-b ya Mkataba

<sup>129</sup> ICTY, Chumba cha rufaa, *Prosecutor v. D. Milosevic*, "Judgement", 12 November 2009, IT-98-29/1-A, par. 290; ICTY, Chumba cha rufaa, *Prosecutor v. Kordic and Cerkez*, "Judgement", 17 December 2004, IT-95-14/2-A, par. 28.

<sup>130</sup> ICTR, Chumba cha rufaa, *Kamuhanda v. The Prosecutor*, "Judgement", 19 September 2005, ICTR-99-54A-A, par. 76.

kufanyika, ao ii)kutenda kitu ao kutokutenda kitu yenyi ilifanya jinai itendeke<sup>131</sup>, c) ile amri ilikuwa na matukio ya moja kwa moja juu ya jinai kufanyika ao kujaribu kufanyika<sup>132</sup>, na d) kwamba mu akili ya mtu huyu alijua kama, kufuatana na ginsi mambo ilikuwa inaendelea, jinai ilipashwa tu kutendeka wakati wa kutimiza amri. Inawezekana mtu huyu alitoa amri yake kwa njia ya mtu mwingine. Si lazima mtu huyu akuwe alitoa ile amri moja kwa moja kwa mtu mwenye alitenda jinai<sup>133</sup>.

64.Chumba inaamua ya kwamba kuko sababu zakutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura alifanya ile matendo katika cheo yenye alikuwa nao wakati wote ule unaotajwa ndani ya ombi ya Prokirere. Alikuwa mkubwa wa kijeshi wa FDLR wakati ule wote<sup>134</sup>. Kama vile ilifasiriwa hapa juu, baFDLR ni kikundi kikubwa kyenye kiko na uongozi yenye kupangwa mzuri na wazi wazi<sup>135</sup>. Sylvestre Mudacumura alikuwa na mamlaka juu ya waaskari wake na alikuwa na uwezo ya kuingiza watu katika ile jeshi, kupatia waaskari wake cheo na kubafukuza katika jeshi na kubapatia malipizi<sup>136</sup>. Uwezo na mamlaka yake juu ya waaskari wa FDLR ilikua inamuruhusu kukatiza waaskari kujitoshia katika jeshi<sup>137</sup>, kuwapatia ruhusa ya kuoa<sup>138</sup> na kuchunguza kila habari walikuwa

<sup>131</sup> ICTR, Chumba cha rufaa, *Karera v. The Prosecutor*, "Judgement", 2 February 2009, ICTR-01-74-A, para. 211; ICTR, Chumba cha rufaa, *Nahimana et al v. The Prosecutor*, "Judgement", 28 November 2007, ICTR-99-52-A, par. 481.

<sup>132</sup> *Lakini angalia* ICTR, Chumba cha rufaa, *Kamuhanda v. The Prosecutor*, "Judgement", 19 September 2005, ICTR-99-54A-A, par. 75; ICTR, Chumba cha rufaa, *Prosecutor v. Kayishema and Ruzindana*, "Judgement (Reasons)", 1 June 2001, ICTR-95-I-A, par. 186.

<sup>133</sup> *Ona* ICTY, Chumba cha kesi, *Prosecutor v. Dordjevic*, "Judgement", 23 February 2011, IT-05-87/1-T, par. 1871; ICTY, Chumba cha kesi, *Prosecutor v. Kordic and Cerkez*, "Judgment", 26 February 2001, IT-95-14/2-T, par. 388; ICTY, Chumba cha kesi, *Prosecutor v. Blaskic*, "Judgment", 3 March 2000, IT-95-14-T, par. 282.

<sup>134</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 11, uk. 5, 10 na 158 ; Ombi ya Prokirere, nyongeza 12, uk. 84 na 85 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 15, uk 97 na 334 ; Ombi ya Prokirere kip 30 ; uk. 182 na 183 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 44, uk. 9 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 46, uk. 3 ; Ombi ya Prokirere, kip 72, uk 34 ; Ombi ya mwesha mashtaka, Uk.. 94, uk. 6 ; Ombi ya prokirere, nyongeza 117, uk. 38 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 118, uk. 89 mpaka 91.

<sup>135</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 13, uk. 94 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 205 ; Ombi ya Prokirere, Uk. 15, uk. 81 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 16, uk. 89. Ombi ya Prokirere, Uk.. 18, uk. 537 mpaka 543 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 19, uk. 170 mpaka 183 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 27, uk. 177 mpaka 179 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 59, uk. 17 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 78, uk. 28 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 27, uk. 158 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 30, uk. 181, 183 na 188 ; Ombi ya Prokirere, Uk.. 39, uk. 185 mpaka 187; Ombi ya Prokirere, Uk.. 94, uk. 6; Ombi ya Prokirere, Uk.. 118, uk. 89;

<sup>136</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 11, uk. 56; Ombi ya Prokirere, Uk.. 12, uk. 366; Ombi ya Prokirere, Uk. 13, uk. 94; Ombi ya Prokirere, Uk.. 15, uk. 81,183 na 214; Ombi ya Prokirere, Uk.. 19, uk. 204; Ombi ya Prokirere, Uk.. 20, uk. 123 na 188; Ombi ya Prokirere, Uk.. 27, uk. 158; Ombi ya Prokirere, Uk. 11, uk. 56;

<sup>137</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 12, uk. 191 mpaka 194; Ombi ya Prokirere, Uk. 21, uk. 646 na 647;

na pokea kutoka inje<sup>139</sup> ao kutoka kwa batu bengine ba mu FDLR<sup>140</sup>. Amri za Sylvestre Mudachumura zilipashwa kabisa kabisa kuheshimika<sup>141</sup>.

65.Chumba inaamini ya kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura alitoa amri kwa watu wengine kusudi ya kufanya operesheni za vita za namna ya pekee. Ni wakati wa zile operesheni njo jinai za kivita zenye Chumba ilihakikisha zilitendeka. Mwanzo wa mwaka 2009, amri moja kubwa kwa jumla ilitolewa chini ya uongozi wa Sylvestre Mudacumura kusudi ya kufanya janga ya kibinadamu<sup>142</sup>. Sylvestre Mudacumura alikubali pia amri ingine kubwa kwa jumla ya kupora vitu ya basivile juu bisaidie kazi za kijeshi za baFDLR<sup>143</sup>. Bikundi ya FDLR byenye bilitumwa ku kiwanja ya operesheni bilifanya operesheni zenye Sylvestre Mudacumura alipanga ao kukubali<sup>144</sup> na inajulikana kwamba operesheni za mkubwa zilipashwa kuruhusiwa na yeye<sup>145</sup>. Kuko sehemu ya ushahidi yenye inaonesha vile vile kama Sylvestre Mudacumura alikubali mashambulio zianzishwe pale Mianga<sup>146</sup> na Busurungi<sup>147</sup>.

66.Kufuatana na hiyo, Chumba inaamini ya kwamba kuko sababu zakutosha za kuamini kwamba amri zenye Sylvestre Mudacumura alitoa zilikuwa na matokeo ya moja kwa moja juu ya jinai zenye Chumba ilisema pale juu kama zinahakikishwa. Uwezo yake yenye inaonekana wazi juu ya batu benye balitenda moja kwa moja zile jinai inahakikisha kwamba amri zake zilikuwa na matokeo ya moja kwa moja ku utendaji wa zile jinai.

<sup>138</sup> Ombi ya Prokirere, kip. 30, uk. 213.

<sup>139</sup> Ombi ya Prokirere, Uk. 30, uk. 213

<sup>140</sup> Ombi ya Prokirere, Uk. 16, uk. 213;

<sup>141</sup> Ombi ya Prokirere, Uk. 13, uk. 94; Ombi ya Prokirere, ku Uk. 19, uk. 206 na 2012; Ombi ya Prokirere, ku Uk. 27, uk. 178.

<sup>142</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 106,107,224 mpaka 226, 269, 284, 287, 353 mpaka 354; Ombi ya Prokirere, Uk.. 16, uk. 417 mpaka 420; Ombi ya Prokirere, Uk.. 19, uk. 232.

<sup>143</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 18, uk. 524,525 na 620 mpaka 640; Ombi ya Prokirere, Uk. 20, uk. 229 na 230; Ombi ya Prokirere, Uk.. 21, uk. 829 mpaka 839.

<sup>144</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 11, uk. 107; Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 113, 125, 126 na 204; Ombi ya Prokirere, Uk.. 16, uk. 91, 92, 117, 118, 166 na 308 mpaka 315; Ombi ya Prokirere, Uk.. 19, uk. 490; Ombi ya Prokirere, Uk.. 21, uk. 393;421, 422, 668, 845 na 848; Ombi ya Prokirere, Uk.. 118, uk. 60 na 61.

<sup>145</sup> Ombi ya Prokirere, kip. 16, uk 166 na 308 mpaka 312 ; Ombi ya Prokirere kip 18 ; uk. 626 na 627 ; Ombi ya Prokirere, kip. 21, uk. 393 ; Ombi ya Prokirere, kip. 118, uk. 60 na 89.

<sup>146</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 13, uk. 138; Ombi ya Prokirere, Uk.. 16, uk. 154 na 155; Ombi ya Prokirere, Uk.. 17, uk. 440 mpaka 443.

<sup>147</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 11, uk. 45; Ombi ya Prokirere, Uk.. 13, uk. 76; Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 113;

Kuheshimu hizo amri yake ya jumla ya kusema kufanyike janga ya kibinadamu nayo ni ushahidi ingine kuhusu ile. Kwa mfano, temwe moja anatambua kama shambulio ya mwezi ya tano 2009 ya Busurungi ilifanyika kwa kuheshimu ile amri<sup>148</sup>.

67.Kwa mwisho, Chumba inaamini ya kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura : i) alifahamu kiukweli hali zote zakuonesha kwamba kulikuwa vita, na ii) alikuwa ana jua vizuri kwamba, kama anatoa amri, wakati wa kutimiza zile amri, kufuatana na ginsi mambo ilikuwa inaendelea, zile jinai zilipashwa tu kutendeka. Kwa upekee, kulikuwa mfumo ya simu ya hajabu sana ili Sylvestre Mudacumura aweze kupokea ripoti kila mara kuhusu operesheni za kijeshi<sup>149</sup>. Alipata habari zenye zinasema kama jinai zilitendeka<sup>150</sup>. Alipata pia habari kama waaskari wenye walikuwa chini ya uongozi wake balishtakiwa kama balifanya jinai zenye bikundi ya kimataifa na bikundi byenye habiko bya kiserikali bilisema<sup>151</sup>.

68.Kuhusu mashambulio ya Mianga na Busurungi ku mwezi ya tano 2009, kuna habari zenye zinasema vile vile kama Sylvestre Mudacumura naye alikuwa mu benye balitafuta kufichika hali kamili ya matendo ya jinai yenye baFDLR balifanya pale<sup>152</sup>. Sylvestre Mudacumura hayaitikaka hata siku moja mbele ya batu kama baaskari bake balifanyaka jinai<sup>153</sup>. Kuna wakati bakomanda bake benye balishtakiwa ya kwamba balifanya jinai balipandishwa cheo kutokana na amri yake<sup>154</sup>.

69.Kutokana na hiyo, Chumba imeona kama kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anabeba, vile inaandikwa mu artikle 25-3-b ya Mkataba, muzigo

<sup>148</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 30, uk. 122;

<sup>149</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 12, uk. 84, 85 na 383; Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 205; Ombi ya Prokirere, Uk.. 16, uk. 117 mpaka 125; Ombi ya Prokirere, Uk.. 19, uk. 205 mpaka 212; Ombi ya Prokirere, Uk.. 20, uk. 123; Ombi ya Prokirere, Uk.. 21, uk. 421, 422, 668 na 689;

<sup>150</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 12, uk. 383; Ombi ya Prokirere, Uk.. 21, uk. 393, 421, 422 na 848; Ombi ya Prokirere, Uk.. 112, uk. 115 na 135.

<sup>151</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 43, uk. 52; Ombi ya Prokirere, Uk.. 44, uk. 202 na 204.

<sup>152</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 4, (pamoja na ushahidi yenye banataja pale).

<sup>153</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 14, uk. 381; Ombi ya Prokirere, Uk.. 17, uk. 797 na 798; Ombi ya Prokirere, Uk. 44, uk. 202 mpaka 204.

<sup>154</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 39, uk. 298.

ya jinai za kivita zenye zilitajwa hapa juu. Chumba inatia mkazo kusema kwamba hii uamuzi haina matokeo ku uamuzi yoyote yenye Chumba inaweza kutoa, mu bipindi bya nyuma bya masambo, kuhusu aina nyingine ya muzigo ya jinai.

#### **IV. Mafaa ya kumufunga Sylvestre Mudacumura kufuatana na artikle 58-1-b ya Mkataba**

70.Chumba inakumbusha kama artikle 58-1 ya Mkataba inalazimisha Chumba kutoa manda ya kukamata kama iko na uhakika ya kwamba kuna sababu zakutosha za kuamini kwamba ule mtu alifanya jinai yenye iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama na kwamba kukamata ule mtu yule inaonekana kuwa ya muhimu kwa kuhakikisha ya kwamba : i) ule mtu atafika mbele ya Mahakama ; ii) ya kwamba ule mtu hatazuia anketete ao masambo mbele ya Mahakama ao kuharibu mwendo wa masambo ; iii) na tena kama ule mtu hataendelea kutenda jinai yenye banamushtakia ao jinai ingine yenye inaambatana nayo, yenye iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, na yenye kutendeka mu hali moya na ile jinai ingine. Kwa kutoa manda ya kukamata, yatosha tu Chumba ione ya kwamba moja ya masharti zenye zinatajwa ku artikle 58-1-b ya Mkataba inaenea.

71.Chumba ilisha sema ya kama kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anaweza kushtakiwa kusema ya kwamba anabeba muzigo ya jinai kutokana na artikle 25-3-b ya Mkataba inayohusu jinai za kivita zilizotajwa hapa juu mu sehemu II-B.

72.Chumba inaona kwamba kukamata Sylvestre Mudacumura ni kwa lazima kwa kuhakikisha ya kwamba atafika mbele ya Mahakama kwa kujitetea dhidi ya mashtaka haya mazito, huko kwenye anazaniwa kama anaishi katika eneo moja ya kujificha ya jimbo

ya Nord-Kivu, huko Kongo na kwenye anapata msaada wa marafiki zake toka inchi mbali mbali. Hii msaada inaweza kumsaidia kuepuka Mahakama<sup>155</sup>.

73. Chumba inaona pia ya kwamba kukamata Sylvestre Mudacumura ni kwa lazima kwa kuhakikisha ya kwamba hatazuia ankete wala masambo mbele ya Mahakama ao kuharibu mwendo wa masambo, kwa sababu : i) anaonekana ya kwamba yeye njo angali na cheo na uongozi ya mkubwa sana ya kijeshi ya FDLR, ii) amekuwa tena na mamlaka zaidi ya uongozi wa kikundi kile kisha kufungwa kwa Callixte Mbarushimana<sup>156</sup>, na iii) iko na vifaa ya hajabu kwa kupata habari kule mu eneo ya mashariki ya Kongo kwenye anapatikana<sup>157</sup>. Na zaidi, Prokirere anasema kama baviktime bamingi, batemwe na batu bengine benye banaweza kuwa batemwe mu hii afere banaishi fasi zenye ziko chini ya uongozi wa FDLR<sup>158</sup>.

74. Mwisho, Chumba inaona ya kwamba kukamata Sylvestre Mudacumura ni kwa lazima kwa kuhakikisha ya kwamba hataendelea tena kutenda jinai zenye ziko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama na zenye kutendeka mu hali sawa sawa na ile yenye ilitajwa, kwa sababu, kwa leo inawezekana kama baFDLR bangali chini ya mamlaka yake na inawezekana walifanya operesheni za kijeshi katika majimbo za Kivu, kiisha mwezi ya kenda 2010<sup>159</sup>.

75. Kutokana na ushahidi yote yenye ilioneshwa, na bila kuzungumzia uamuzi yenye itaweza kuchukuliwa nyuma kufuatana na artikle 60 ya Mkataba na Kanuni 119 ya Kanuni za Utaratibu na Ushahidi, Chumba inaamua ya kwamba kukamatwa kwa Sylvestre Mudacumura ni kwa lazima kufuana na aya i), ii) na iii) za artikle 58-1-b ya Mkataba.

---

<sup>155</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 88, Ombi ya Prokirere, Uk.. 74, uk. 24 mpaka 30; Ombi ya Prokirere, Uk. 94, uk. 6.

<sup>156</sup> Ombi ya Prokirere, Uk. 56, uk. 128 na 129; Ombi ya Prokirere, Uk.. 94, uk.6.

<sup>157</sup> Ona juu uk. 67

<sup>158</sup> Ombi ya Prokirere, Uk.. 89.

<sup>159</sup> Ombi ya Prokirere, Uk. 89; Ombi ya Prokirere, Uk.. 9, uk. 56 mpaka 59 (Maoni ya Baraza la Usalama ya Umoja wa Mataifa ya tarehe 29 novemba 2011 inayoomba baFDLR waweka silaa yote chini na “waache mara moja kutenda ma ukali na kukiuka haki za binadamu dhidi ya basivile wa Kongo DRC”).

## V. Kwa kumaliza

76. Kufuatana na yote yenye imeandikwa hapa juu, Chumba inaamini kwamba kuko sababu za kutosha za kuamini kwamba Sylvestre Mudacumura anabeba muzigo ya jinai, vile inaandikwa ku artikle 25-3-b ya Mkataba, kwa ajili ya jinai za kivita zilizotendeka tangu tarehe 20 mwezi wa kwanza 2009 mpaka mwisho wa mwezi ya kenda 2010 kama vile zinaandikwa katika nukta 30 mpaka nukta 58 za hii uamuzi.

77. Chumba inaamua, kufuatana na artikle 58-1 ya Mkataba, kutoa manda ya kukamata Sylvestre Mudacumura.

78. [IMEVUTWA]<sup>160</sup>.

79. [IMEVUTWA].

---

<sup>160</sup> [IMEVUTWA].



## KWA SABABU HIZI, CHUMBA

### INAAMUA

ya kwamba afere ya Sylvestre Mudacumura iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama na kwamba manda ya kukamata mtu huyu inaonekana kuwa ni ya lazima kutokana na muzigo ya jinai anabeba, vile inaandikwa mu artikle 25-3-b ya Mkataba, na kufuatana na kanuni yenye inatumikish, mu jinai zenye zilitendeka mu majimbo za Kivu huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo tangu tarehe 20 mwezi wa kwanza 2009 mpaka mwisho wa mwezi ya kenda 2010, kama vile imeandikwa ku nukta 30 mpaka 58 za hii uamuzi :

- i) Jinai za kivita za mauaji ( artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 2) ;
- ii) Jinai za kivita za kukata viungo ya mwili (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 4);
- iii) Jinai za kivita za utendeaji wa kikatili (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 6) ;
- iv) Jinai za kivita za mateso (artikle 8-2-c-i ya Mkataba, shtaka 9) ;
- v) Jinai za kivita za kuvunjia mtu heshima (artikle 8-2-c-ii ya Mkataba, shtaka 14) ;
- vi) Jinai za kivita za shambulio dhidi ya basivile (artikle 8-2-e-i ya Mkataba, shtaka 1) ;
- vii) Jinai za kivita za uporaji (artikle 8-2-e-v ya Mkataba, shtaka 12) ;
- viii) Jinai za kivita za ubakaji (artikle 8-2-e-vi ya Mkataba, shtaka 7) ;
- ix) Jinai za kivita za kubomoa vitu (artikle 8-2-e-xii ya Mkataba, shtaka 11) ;

### INAFANYA, KUTOKANA ILE, MANDA YA KUKAMATA

Sylvestre Mudacumura, aliyezaliwa mwaka 1954 mu *cellule* ya Ferege, *secteur* ya Gatumba mu mtaa wa Kibilira, mu *préfecture* ya Gisenyi, pale Rwanda. Anajulikana pia kwa majina

ya Pierre Bernard Mupenzi, kamanda Pharaon, Pharaon, Mudac, Mukanda na Radja ; wakati ya utendaji ya jinai na pia siku Prokirere alileta ombi yake, Sylvestre Mudacumura alikuwa kiongozi mkubwa sana kuliko wote wa jeshi ya *Forces démocratiques pour la libération du Rwanda*,

## INAAMURU GREFYE

1) kutayarisha na kutuma kwa wakubwa wa serkali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ombi ya uhusiano kwa ajili ya kukamata na kutoa Mudacumura kwa Mahakama, na hii kisha kuongea na kusaidiana na Prokirere; ombi hii inapashwa kuwa na habari zote na vikartasi kama vile inaombwa katika artikle 89-1 na 91 ya Mkataba na pia katika Kanuni 176-2 na 187 za Kanuni za Utaratibu na Ushahidi (« Kanuni »);

2) kutayarisha na kutumia kila nchi yenye inayohusika kila ombi ya kukamata na ya kutoa ya zaidi ambayo inaweza kuwa ya lazima juu ya kukamata Sylvestre Mudacumura na kumtoa kwa Mahakama, kufuatana na artikle 89 na 91 za Mkataba;

3) kutayarisha na kutuma, kama hali inaomba hivi, ombi ya kukamata kwa muda kufuatana na artikle 92 ya Mkataba;

4) kutayarisha na kutuma kwa kila inchi inayohusika, kufuatana na artikle 89-3 ya Mkataba, ombi yoyote ya kupita ambayo ni ya lazima juu ya kutoa Sylvestre Mudacumura kwa Mahakama ;

5) kuhusiana na Prokirere juu ya kuomba Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Ufalme wa Uholanzi ziombe Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Baraza la Umoja wa Nchi za Ulaya ziondowe kwa muda kikwazo ya kusafiri ya Sylvestre Mudacumura juu mtu huyu aweze kutolewa kwa Mahakama na akubalike kuingia Uholanzi ;

[IMEVUTWA]; na

**INAOMBA PROKIRERE**

1) kujulisha Chumba na Grefye, kadiri inaruhurisiwa na mapashwa yake ya kulinda siri, habari zote zenye iko nazo zenye zinawezesha kuepusha baviktime ao batemwe hatari yenye inaweza kutokana na maombi ya uhusiano yenye imetajwa hapa juu; na

2) kujulisha Chumba na Grefye, kadiri inaruhurisiwa na mapashwa yake ya kulinda siri, habari zote zenye iko nazo zenye, kwa kuona yake, zinaweza kurahisisha kutuma na kutimiza maombi ya uhusiano yenye imetajwa hapa juu.

Inafanyika kwa Kiingereza na Kifaransa, maandiko ya Kiingereza njo ya kuaminika kuliko ingine.

*/saini/*

---

**Bibi jije Ekaterina Trendafilova**  
**Jije prezida**

*/saini/*

---

**Bw. jije Hans-Peter Kaul**

*/saini/*

---

**Bw. jije Cuno Tarfusser**

Imefanyika siku ya tano tarehe 13 mwezi ya saba 2012  
pa La Haye (Uholanzi)